*Re-aranged and translated by Pastor Stephen Letta*

**Paulo Saburi Kilonzo, (1890-1979)**

Paulo Saburi Kilonzo, Mpare (Mwasu), alizaliwa mwaka 1890 huko Suji – Gonjanza. Paulo Saburi Kilonzo alikuwa kiongozi bora wa kiroho miongoni mwa Waadventista nchini Tanzania na Kenya, na ni mmoja wa Watanzania wawili wa kwanza kutawazwa kuwa mchungaji katika Kanisa la Waadventista Wasabato.

Baba yake aliitwa Kilonzo Mrekwa na mama yake Kahindi Kajiru. Kwa vile baba yake Kilonzo alitoka katika familia ya watawala wa jadi, aliteuliwa kuwa kuhani mkuu wa kimila na alihudumu katika sherehe kuu za kidini. Pia alisimamia mambo ya mungu wa vita, Murungu wa Gu , kama alivyofahamika na watu wa kabila lake la Kipare na kila kulipokuwa na vita alikuwa akiongoza kundi la wapiganaji kumlinda mungu huyo dhidi ya maadui.

Ndugu wawili wa Kilonzo, Yohana Bwelela Kilonzo na Sangiwa Eliamani Kilonzo, wakawa wainjilisti wa Kanisa la Waadventista Wasabato.

## KUBATIZWA

Kilonzo alibatizwa Juni 27, 1914 na alikabili upinzani mkali kutoka kwa baba yake. Aliitwa kufanya kazi ya ualimu Februari 1916 huko Ntambwe. Wakati wa Vita vya Kwanza vya Ulimwengu, aliwekwa kizuizini na Waingereza mnamo Agosti na Septemba 1917 pamoja na kikundi cha walimu wa Wapare, lakini baadaye waliachiliwa na kuendelea na shughuli zao za kanisa kwa siri. Ufundishaji ulianza tena mwaka wa 1919, wakati Waingereza waliporuhusu, na Kilonzo alichaguliwa kufundisha watoto wa washiriki wa kanisa huko Suji.

## KUFUNGA NDOA

Kilonzo alifunga ndoa Aprili 1920. Wakati huo, tayari alikuwa kiongozi wa kanisa anayetegemewa kwa sababu, mwaka wa 1921, Waadventista wa Pare, ambao hawakuwa na mmishonari tangu 1919, walimtuma kwenda kituo cha misheni cha Gendia, kulipokuwa makao makuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato nchini Kenya akiandamana na Ezekiel Mbwana, aliyekuwa mzee wa kanisa kiongozi wa makundi manne ya Waadventista yaliyokuwa yamepangwa huko Pare Kusini.

## MHUDUMU WA ELIMU YA WATU WAZIMA

Mnamo 1922 na 1923, Kilonzo alihudumu katika mradi wa elimu ya watu wazima kwa washiriki wa kanisa, na mnamo 1923 alitawazwa kuwa mzee wa kanisa katika kanisa la Mamba, kanisa la Waadventista lililokuwa na nguvu zaidi katika Milima ya Pare wakati huo. Mnamo 1924, alifungua shule mpya huko Mamba – Myamba. Mnamo mwaka 1925 alianza kazi ya umishonari katika Milima ya Usambara, hasa miongoni mwa Wapare

waliokuwa wameishi huko. Akiwa na kundi la watu wengine wanane, alikuwa miongoni mwa Waadventista Wazazi wa kwanza kuhitimu na cheti cha ualimu wa serikali ya Daraja la III kutoka Shule ya Ualimu ya Suji mnamo 1927.

**MWINJILISTI WA VITABU**

Baada ya kupewa leseni ya utumishi mwaka wa 1928, Kilonzo aliteuliwa kuwa mkurugenzi wa idara ya uchapishaji ya East Tanganyika Field – jukumu ambalo alilifanya kwa uhodari mkubwa katika kanisa hili changa. Akiwa katika nafasi hii, alikuwa sehemu ya timu ya watu wanne iliyojaribu kufikia Zanzibar kwa kuuza vitabu vya kidini. Waliuza mamia ya vitabu na vijizuu kwa siku tatu na kusababisha mtafaruku mkubwa katika jamii ya Waislamu. Wengine walitaka vitabu hivyo vizuiwe, huku wengine wakipendezwa na ujumbe wa Kikristo. Mbali na mradi huu wa Zanzibar, Kilonzo pia aliuza vitabu Tanga, Morogoro, Dodoma, Singida, Lindi, Arusha, na katika eneo la Moshi hadi 1933. Shughuli hizi zilikuwa za kipekee kabisa katika Afrika Mashariki katika kipindi hicho cha awali.

Mnamo 1929, Kilonzo alitumwa Dar es Salaam, ambako aliuza vitabu pamoja na Esikia Wandea Kirekero hadi 1931. Hata hivyo, soko la vitabu halikuwa la kuridhisha, na lengo la kuanzisha jumuiya ya Waadventista katika mji mkuu halikufaulu. Juhudi za kusambaza vitabu ziliweza kumuongoa muongofu mmoja tu ambaye ni Jim Mkonkwe, ambaye hatimaye alirejea katika nchi yake ya asili ya Malawi. Kilonzo alirudi nyumbani mapema kwa sababu mkewe alikuwa na matatizo ya kiafya.

**KUWEKWA WAKFU**

Kilonzo aliwekwa wakfu mwaka 1932 na Elisa Manongi Kilonzo, miaka tisa kabla ya Watanzania wengine kuwekwa wakfu kuwa wachungaji wa Kanisa la Waadventista Wasabato katika maeneo ya Ziwa Victoria, mkoa mwingine wenye waumini wengi Waadventista. Utumishi wake kama mhudumu katika Milima ya Pare kuanzia 1934 hadi 1939 ulijumuisha pia majukumu mengine maalum kama vile safari za uchunguzi kati ya Wamasai na eneo la Moshi, ambapo viongozi wa wamishonari walitaka kuanzisha shughuli za injili. Uwezo wake wa kushughulikia kazi hizo zenye changamoto pengine ulichangia kuteuliwa kwake kama kaimu mkurugenzi wa misheni huko Mbeya mwaka wa 1939 wakati mmishonari Mjerumani Rudolf Reider alipolazimika kurudi Ujerumani kwa sababu ya vita. Kilonzo, hata hivyo, alisitasita kuhudumu katika eneo hilo la mbali na alikubali kazi hiyo mwaka wa 1940. Alifanya kazi huko hadi 1943 na kisha kuhamishiwa Utimbaru karibu na Ziwa Victoria, ambako alitumikia kati ya Wakuria na Wajaluo hadi 1947 na kushiriki katika ufunguzi wa makundi.

## ATUMWA KENYA

Baada ya uzoefu huu wa kimishionari nchini Tanzania, kipindi kingine kama mchungaji wa Suji na sehemu ya magharibi ya Milima ya Pare Kusini, na kipindi kifupi kama katibu mchapishaji wa Tanganyika Mission Field mwaka 1951 na 1952 –akawa Mwafrika wa kwanza kushikilia wadhifa mkubwa wa kitaifa wa kanisa kama huo. Kilonzo aliendesha kazi ya Waadventista miongoni mwa Wakisii wa magharibi mwa Kenya, kuanzia 1954 hadi 1958. Kufikia 1955, alikuwa katika usimamizi wa washiriki 341 katika makanisa mawili pamoja na zaidi ya 100 katika kila darasa la waliovutiwa na la ubatizo. Mwishoni mwa huduma yake, idadi ya makanisa iliongezeka hadi sita.

Kufikia 1959, alipaswa kustaafu lakini akachagua kuendelea kumtumikia Mungu kwa bidii. Kanisa lilimtuma kuongoza Misheni ya Changamwe karibu na Mombasa, ambayo ilikuwa imeanzishwa mwaka wa 1934 lakini haikuwahi kupata mafanikio mengi. Kupitia huduma yake, idadi ya waumini iliongezeka kutoka watano hadi ishirini na tano. Mnamo 1961, Kilonzo aliitwa kuongoza kazi katika Mtaa wa Kamba katikati mwa Kenya ambako alitatua matatizo makubwa ya ndani.

## AREJEA TANZANIA

Mwaka 1963 alifanya kazi katika kituo kipya kilichofunguliwa Moshi. Huko aliongoza njia ya kuuza vitabu vya Kikristo, kufanya kazi na wachungaji wa Kilutheri na kuanzisha uhusiano mzuri na Askofu Stefano Moshi. Wakati wa utumishi wake huko hadi mwaka 1967, vikundi kumi na vinne vya Shule ya Sabato vilijitokeza katika mtaa huu ambayo ni pamoja na maeneo ya Moshi na Arusha. Uteuzi wake wa mwisho ulikuwa Makanya na Hedaru, chini ya Milima ya Pare, hadi 1972.

Huduma ndefu ya Kilonzo inamfanya kuwa mwakilishi wa vizazi viwili vya viongozi wa kanisa. Akiwa na Waadventista wengine wa mapema wa Kitanzania ambao pia walihudumu kama wamisionari katika mikoa mingine nchini Tanzania na kwingineko, anawakilisha kizazi cha kwanza cha viongozi wa Kiadventista wa Kitanzania na nguvu ya kimisionari iliyotoka kwenye makanisa ya vijana ya Pare Kusini. Huku viongozi wengine wachache wakishiriki majukumu ya idara ya Tanganyika Mission Field katika miaka ya 1950, Paulo Kilonzo ni wa kizazi cha kwanza cha viongozi wa kitaifa wa Waadventista. Walilipa kanisa hilo utambulisho ambao ulienda umbali mrefu zaidi ya kanisa mahalia la Waadventista katika tabia na ambalo wakati huo lilikuwa halitawaliwi tena na mifumo ya Wazungu. Atakumbukwa kwa shauku yake ya kuhudumu na nia yake ya kufanya kazi hata mbali na nyumbani kwake.